TANGAZO LA SERIKALI NO. 804 la tarehe 28/12/2018

# SHERIA YA MAJISAFI NA USAFI WA MAZINGIRA
(SURA. 272)

## AMRI

*(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (1)(d)*

AGIZO LA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA ARUSHA ("ARUSHA WSSA"), LA KUREKEBISHA BEI ZA HUDUMA ZA MAJI SAFI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2018

Kichwa cha Agizo

1. Agizo hili litajulikana kama, Agizo la Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Arusha ("Arusha WSSA"), (la Kurekebisha Bei), la Mwaka 2018.

Tarehe ya Kuanza

2. Agizo hili litaanza kutekelezwa rasmi kuanzia tarehe 1 Disemba 2018 mpaka 30 Juni 2021.

Marekebisho ya Bei

3. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Arusha WSSA zinarekebishwa kulingana na Jedwali la Kwanza katika Agizo hili.

Masharti

4. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:
   (a) Ifikapo tarehe 31 Machi 2019 au kabla, Arusha WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara uliopitiwa upya kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;
   (b) Arusha WSSA, itawawekea dira wateja ambao wana vyanzo vyao vya maji ili kuweza kupata msingi wa kupanga bei ya majitaka;

(c) Arusha WSSA itaandaa mpango wa kuwaelimisha wateja kuhusu shughuli zake na umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji. Mpango huo uwasilishwe EWURA kabla au ifikapo tarehe 31 Machi 2019 kwa mapitio na kudhibitishwa kabla ya kuanza utekelezaji wake;

(d) Arusha WSSA itatekeleza miradi kwa kutumia fedha za ndani kama ilivyo katika Jedwali la pili la Agizo hili;

(e) Arusha WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu la Agizo hili;

(f) Arusha WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa; na

(g) Arusha WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Arusha WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za majisafi na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Arusha WSSA katika siku zijazo.

Agizo Na. 2016 -003 la tarehe 1 February 2016 linafutwa

5. Agizo hili linatengua Agizo la Marekebisho ya Bei Na. 2016 -003 la tarehe 1 February 2016 katika maeneo yanayohudumiwa na Arusha WSSA.

______

Majedwali

______

JEDWALI LA KWANZA: BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali Namba 1(a): Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

| Kundi la Wateja | Matumizi kwa Uniti | Bei za Sasa | Bei Zilizopendekezwa | | | Bei Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 0 to 5 | 1,030 | 1,236 | 1,390 | 1,248 | 1,170 | 1,330 | 1,510 |
| | >5 <15 | 1,200 | 1,440 | 1,620 | 1,455 | 1,360 | 1,550 | 1,750 |
| | >15 | 1,400 | 1,679 | 1,890 | 1,697 | 1,590 | 1,810 | 2,050 |
| Taasisi | | 1,168 | 1,402 | 1,577 | 1,417 | 1,330 | 1,510 | 1,710 |
| Biashara | | 1,492 | 1,790 | 2,014 | 1,809 | 1,700 | 1,930 | 2,180 |
| Viwanda | | 1,982 | 2,377 | 2,676 | 2,402 | 2,250 | 2,560 | 2,900 |
| Magati | | 780 | 936 | 1,053 | 945 | 1,000 | 1,000 | 1,000 |
| Viwanda vya Maji ya Chupa | | 11,830 | 14,192 | 15,969 | 14,339 | 13,450 | 15,300 | 17,290 |
| Weighted Average Tariff | | 1,361.56 | 1,633.46 | 1,837.95 | 1,650.37 | 1,548.56 | 1,759.34 | 1,989.25 |

Jedwali Namba 1(b): Tozo ya Huduma ya Sasa na Iliyoidhinishwa (Shilingi/Mwezi)

| Customer Category | Tozo ya Sasa | Tozo Zinazopendekezwa | | | Tozo Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/ | 2019/ | 2020/21 | 2018/ | 2019/ | 2020/21 |
| Majumbani | 2,200 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Taasisi | 3,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Biashara | 3,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Viwanda | 5,500 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

Jedwali Namba 1(c): Bei za Sasa, Zilizopendekezwa na Zilizoidhinishwa za Majitaka (Shilingi/uniti)

| Customer Category | Bei za Sasa | Bei Zinazopendekezwa | | | Bei zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 330 | 360 | 390 | 420 | 355 | 375 | 395 |
| Taasisi | 450 | 500 | 550 | 600 | 480 | 510 | 540 |
| Biashara | 660 | 710 | 760 | 810 | 705 | 750 | 790 |
| Viwanda | 770 | 820 | 870 | 920 | 820 | 870 | 920 |

Jedwali Namba 1(d): Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Kurejeshewa Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Kurejeshewa Huduma)

| Kundi la Wateja | Ada ya Sasa | Ada Zilizopendekezwa | | | Ada Zilizoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majumbani | 15,000 | 16,000 | 17,000 | 18,000 | 15,000 | 15,000 | 15,000 |
| Taasisi | 19,000 | 20,000 | 21,000 | 22,000 | 19,000 | 19,000 | 19,000 |
| Biashara | 20,000 | 21,000 | 22,000 | 23,000 | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| Viwanda | 26,000 | 27,000 | 28,000 | 29,000 | 26,000 | 26,000 | 26,000 |

Jedwali Namba 1(e): Ada ya Sasa, Inayopendekezwa na Iliyoidhinishwa ya Huduma ya Boza kwa Majisafi na Uondoaji wa Majitaka (Shilingi/Ukubwa wa Boza)

| Ujazo kwa lita | Ada ya Sasa | Ada Inayopendekezwa | | | Ada Iliyoidhinishwa | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Majisafi 10,000 | NA | 106,000.00 | 112,360.00 | 119,101.60 | 106,000 | 112,400 | 119,100 |
| Majisafi 5,000 | NA | 84,800.00 | 89,888.00 | 95,281.28 | 89,000 | 89,900 | 95,200 |
| Majitak | NA | 84,800.00 | 89,888.00 | 95,281.28 | 89,000 | 89,900 | 95,300 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| a 10,000 | | | | | | | |
| Majitaka 5,000 | NA | 68,900.00 | 73,034.00 | 77,416.04 | 69,000 | 73,000 | 77,400 |

JEDWALI LA PILI
MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA KWA KUTUMIA MAPATO YA NDANI YATOKANAYO NA BEI (SHILINGI KWA MILIONI)

| | 2018/19 | | 2019/20 | | 2020/21 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Jumla |
| Kukarabati vyanzo wa maji vya chemchem vya Olgilai, Ngarendolu na Machare Springs | - | - | - | 165.00 | - | 165.00 | 330.00 |
| Kukarabati na kusafisha visima virefu vya Maji vitano (5) | - | 128.33 | - | 299.64 | - | 448.52 | 876.49 |
| Kujenga na kuendeleza visima virefu viwili vilivyochumbwa eneo la Magereza vyenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 1100 kwa siku. | 374.00 | - | - | - | - | - | 374.00 |
| Kulipa fidia kwenye njia za kupita mabomba makuu ya maji na maeneo ya ujenzi wa miundombinu mingine. | 1,500.00 | - | 2,750.00 | - | 10,750.00 | - | 15,000.00 |
| Kubadilisha na kuweka pumpu kumi na nne (14) za kusukuma dawa ya kutibu maji (chlorine | - | 90.00 | - | 72.00 | - | - | 162.00 |

| | 2018/19 | | 2019/20 | | 2020/21 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Jumla |
| dosing pumps) kwenye vituo vya Sekei, Oligilai, Ngarendolu, Machare, Ilkiurei, Midawe, Themi Hill, Kimaseki, Kilimani, Tembo Club na Burka. | | | | | | | |
| Kukarabati na kubadilisha mitambo na vifaa vya maabara ya Maji (*Digital titrator, CTR, Working bench, Filtration na distillation unit* ). | - | - | - | 35.00 | - | 35.00 | 70.00 |
| Kufanya ukarabati mkubwa (kupaka plasta upya na kubadilisha valvu) kwenye tanki la Maji karibu na hospitali ya “*Mount Meru Hospital*”. | - | - | - | 140.00 | - | - | 140.00 |
| Kubadilisha “Compressor” yenye mgandamizo wa *“66 bars”* | - | - | - | 35.00 | - | - | 35.00 |
| Kubadilisha valvu 28 ambazo hazifanyi kazi kwenye “*Break Pressure Tanks (BPTs)”* | - | 28.00 | - | - | - | - | 28.00 |
| Kibadilisha pampu tisa (9) kwenye visima virefu vya Ilkiurei, Kiranyi I, Old Sanawari, | - | 133.33 | - | 133.33 | 133.33 | - | 400.00 |

| | 2018/19 | | 2019/20 | | 2020/21 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Jumla |
| Loruvani yard, Sekei, Sombetini, Olgilai, Machare na Magereza . | | | | | | | |
| Kununua na kufunga dira mpya za wateja 51,000 zenye ukubwa wa 1/2" na 3/4". (6,000-2018/19, 15,000 -2019/20, na 30,000- 2020/21) | 480.00 | - | 1,200.00 | - | 2,550.00 | - | 4,230.00 |
| Kujenga chemba 1,875 za dira za maji | 375.00 | - | 600.00 | - | 1,775.00 | - | 2,750.00 |
| Kuhamisha dira 15,000 kwenda kwenye chemba. | 113.74 | - | 56.87 | - | 170.61 | - | 341.22 |
| Kufunga sili kwenye dira za maji 30,000. | 25.00 | - | 25.00 | - | 25.00 | - | 75.00 |
| Kuondoa mlindikano wa mabomba "*Spaghetti*" yenye urefu wa kilomita 100 maeneo ya Unga Limited, Olmatejoo, Uswahilini, Baraa na Moshono | 160.00 | - | 80.00 | - | 80.00 | - | 320.00 |
| Kubadilisha na kufunga valvu na valvu chemba 30 kwenye mtandao wa maji. | - | 10.00 | - | 5.00 | - | 5.00 | 20.00 |
| Kubadilisha mabomba ya maunganisho ya maji yenye kilomita 233. | - | 150.00 | - | 160.00 | - | 170.00 | 480.00 |

| | 2018/19 | | 2019/20 | | 2020/21 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Jumla |
| Kubadilisha na kufunga "*fire hydrants*" 84 | - | 25.00 | - | 25.00 | - | 25.00 | 75.00 |
| Kubadilisha vifaa vya matengezo ya mfumo wa majitaka "*power rodding machine*" | - | 15.00 | - | - | - | - | 15.00 |
| Kufunga dira za maji za malipo ya kabla 3000 "*pre-paid water meters*" | 150.00 | - | 300.00 | - | 450.00 | - | 900.00 |
| Kubadilisha samani na viungio | - | 20.22 | - | 21.43 | - | 22.72 | 64.37 |
| Kununua na kufunga mfumo wa dira za malipo ya kabla "Prepaid meters system" | - | - | 50.00 | - | - | - | 50.00 |
| Kununua and kufunga mfumo wa usimamizi wa taarifa za dira za Maji "*meter management information system*" | - | - | 53.00 | - | - | - | 53.00 |
| Kununua na kufunga mfumo wa Ukaguzi wa Ndani. | | - | 7.50 | - | - | - | 7.50 |
| Kununua na kubadilisha kompyuta 20 kila mwaka | - | 36.00 | - | 38.16 | - | 40.45 | 114.61 |
| Kununua na kubadilisha mashine 12 za kuchapisha na kudurufu *(printers/photocopiers)* | - | 7.01 | - | 7.43 | - | 7.88 | 22.32 |
| TOTAL | 3,177.74 | 642.89 | 5,122. | 1,137.0 | 15,933 | 919.57 | 26,933 |

| | 2018/19 | | 2019/20 | | 2020/21 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| MAELEZO | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Miradi Mipya | Miradi ya Ukarabati | Jumla |
| | | | 37 | 0 | .94 | | .51 |

JEDWALI LA TATU
VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2018/19 – 2020/21)

| Description | Uniti | Lengo la Utendaji | | |
|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 |
| Idadi ya wateja wapya wa majisafi | No. | 6,000 | 15,000 | 30,000 |
| Idadi ya wateja wapya wa majitaka | | 367 | 800 | 1300 |
| Kiwango cha upotevu wa maji | % | 36% | 32% | 29% |
| Wateja wenye Dira | % | 100 | 100 | 100 |
| Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato | % | 95% | 96% | 96% |

Dodoma
......................, 2018

NZINYANGWA E. MCHANY
*Mkurugenzi Mkuu*